Wizara Maswala Ya Haki Ya Marekani
Kitengocha Haki Za Kiraia
Idara Ya Haki Za Wahamiaji Na Waajiriwa

# Macluumaadka Qaxootiga iyo Magangelyo ee Ku saabsan Form I-9

Kila mtu anayeanza kazi kama mfanyakazi nchini Marekani hujaza Form I-9, fomu ya serikali ambayo waajiri hutumia kuthibitisha utambulisho wako na ruhusa ya kufanya kazi.

Hati hii imekusudiwa kukusaidia wewe, wahamaji na wakimbizi, kujaza Form I-9 na kujua haki zako katika mchakato huu. Waajiri wanaokubagua kulingana na uraia wako, hali ya uhamaji au asili ya kitaifa wakati wa mchakato wa Form I-9 wanaweza kukiuka sehemu ya Sheria ya Uhamaji na Uraia INA (Immigration and Nationality Act, INA). Sheria hii ya kupinga ubaguzi inapatikana kwenye 8 U.S.C § 1324b.

**Kwa Section 1 ya Form I-9, toa maelezo kukuhusu.**
Weka jina lako na maelezo mengine kukuhusu Section 1 ya Form I-9. Unaweza kumwomba mtu akusaidie kujaza sehemu hii. Ni lazima utie alama kwenye kisanduku kinachoonyesha hali inayokupa ruhusa ya kufanya kazi. Wakimbizi na wahamiaji wanachukuliwa kuwa“aliens authorized to work” (wageni walioidhinishwa kufanya kazi), kwa hivyo tia alama kwenye kisanduku hiki. Kuna nafasi ya tarehe ya mwisho wa matumizi kando ya kisanduku hiki. Kwa sababu muda wa haki yako ya kufanya kazi hauishi, andika “N/A” (ambayo ina maana "haitumiki") katika nafasi ya tarehe ya muda kuisha.

**Kwa Section 2 ya Form I-9, onyesha hati za mwajiri wako zinazoonyesha utambulisho wako na ruhusa ya kufanya kazi.**
Form I-9 ina orodha tatu za hati ambazo unaweza kuonyesha kwa Section 2 ya Form I-9: List A (hati zinazoonyesha utambulisho wako na ruhusa ya kufanya kazi), List B (hati zinazoonyesha utambulisho wako), na List C (hati zinazoonyesha ruhusa ya kufanya kazi). Ni lazima umuonyeshe mwajiri wako chaguo lako la hati moja ya List A au mchanganyiko wa hati moja ya List B na hati ya List C. Chini ya Form I-9 instructions (maagizo ya Form I-9), baadhi ya hati, zinazojulikana kama receipts (risiti), pia zinakubalika kwa Form I-9 kwa muda tofauti.

Una haki ya kuchagua hati zinazokubalika unazotaka kuonyesha kutoka kwa Form I-9 Lists of Acceptable Documents (Orodha ya Hati Zinazokubalika za Fomu I-9). Mwajiri wako haruhusiwi kukuhitaji uonyeshe hati maalum kulingana na hali yako kama mkimbizi au mhamaji au kulingana na asili yako ya kitaifa. Mwajiri anayehitaji hati maalum anaweza kuwa anabagua kinyume na sheria. Kwa mfano, ingawa unaweza kuwa na Hati ya Uidhinishaji wa Ajira (Employment Authorization Document, EAD), unaweza kuamua kuonyesha hati nyingine badala yake, kama vile kitambulisho cha serikali (hati ya List B) na kadi ya Ruzuku ya Serikali isiyo na kikomo (hati ya List C).

**Unaweza kuwa na aina kadhaa za hati zinazokubalika za Form I-9.**
Unaweza kuonyesha I-94 kwa Form I-9. Utapata kadi yako ya I-94, au unaweza kuchapisha I-94 yako kutoka kwa tovuti ya Customs and Border Protection (Forodha na Ulinzi wa Mipaka).

Ikiwa wewe ni mkimbizi, I-94 ni receipt (risiti) kwa hati ya List A ambayo ni halali kwa siku 90 kutoka siku yako ya kwanza ya kazi. Baada ya siku 90, lazima uonyeshe mwajiri wako ama EAD au mchanganyiko wa hati ya List B na kadi ya Ruzuku ya Serikali isiyo na kikomo.

Ikiwa wewe ni mhamaji, unaweza kutumia I-94 kama hati ya kudumu ya List C ambayo muda wake hauishi.

Wahamiaji na wakimbizi wanastahiki kupata EAD. Ikiwa muda wa EAD yako umeisha lakini umetuma ombi la kubadilisha EAD yako, unaweza kuendelea kufanya kazi na EAD yako iliyopo. Kwa hadi muda wa hadi siku 540 baada ya tarehe ya EAD kuisha muda, unaweza kuendelea kufanya kazi kwa kumwonyesha mwajiri wako EAD yako na notisi ya risiti ya I-797C (ikionyesha kwamba serikali ilipokea ombi lako la kubadilisha EAD). Pigia Sehemu ya Haki za Wakimbizi na Wafanyakazi (Immigrant and Employee Rights Section, IER) simu kwa maelezo zaidi kuhusu upanuzi wa kiotomatiki wa EAD.

Unaweza pia kuonyesha risiti za hati zilizopotea, kuharibika, au kuibiwa.

Pindi tu unapoonyesha hati zako za kukamilisha Form I-9, mwajiri wako anaruhusiwa kukuuliza hati tena katika hali chache tu. Sheria za wakati mwajiri lazima aombe hati tena zinajadiliwa katika Handbook for Employers M-274 (Kitabu cha Mwongozo wa Waajiri M-274).

Ikiwa ulionyesha EAD yako kwa Section 2, mwajiri wako ataomba kuona hati nyingine kufikia wakati muda wa EAD yako unaisha ili kukamilisha Section 3 ya Form I-9. Katia hatua hii, unaweza kuchagua kuonyesha hati moja ya List A au hati moja ua List C, kama vile kadi ya Ruzuku ya Serikali isiyo na kikomo. Unaweza kuchagua kuonyesha EAD mpya, lakini si lazima.

Iwapo ulionyesha kadi ya Ruzuku ya Serikali isiyo na kikomo kwa Section 2 kama uthibitisho wa ruhusa yako ya kufanya kazi na ukaweka “N/A” kwa tarehe ya muda kuisha kando ya “alien authorized to work” (mgeni aliyeidhinishwa kufanya kazi) katika Section 1, mwajiri wako haruhusiwi kukuomba utoe hati zaidi. Waajiri wanaoomba hati kulingana na hali yako kama mhamaji au mkimbizi au kulingana na asili yako ya kitaifa wakati hawahitajiki wanaweza kukiuka sheria. Piga IER simu kwa maelezo zaidi kuhusu wakati mwajiri wako anaruhusiwa kukuomba utoe hati zaidi.

Unaweza kufanya kazi unaposubiri nambari yako ya Ruzuku ya Serikali.
Ukipata kazi lakini huna nambari yako ya RuzUku ya Serikali (Social Security number, SSN) bado, the Usimamizi wa Ruzuku ya Serikali unawaagiza waajiri kwamba wafanyakazi wanaruhusiwa kufanya kazi wakisubiri SSN yao.

Lazima mwajiri wako akulipe kila wakati kwa kazi yoyote iliyokamilika, hata kama bado unasubiri SSN yako.

Iwapo huna SSN yako unapoanza kazi yako, acha wazi kisanduku cha SSN katika Form I-9 ya Section 1.

Iwapo mwajiri wako hutumia E-Verify, E-Verify huagiza waajiri kuchelewesha kuunda kesi ya E-Verify hadi utakapopokea SSN yako. Unaweza kufanya kazi wakati huu ikiwa umekamilisha Form I-9. Sheria za E-Verify rules huruhusu ubaguzi huu haswa na huwapa waajiri maagizo ya kuunda kesi. Maelezo zaidi yanapatikana katika www.e-verify.gov.

*Tazama ukurasa unaofuata*

**Pigia Sehemu ya Haki za Wakimbizi na Wafanyakazi**

(Immigrant and Employee Rights Section, IER)

Laini ya Moja kwa Moja ya Mfanyakazi **1-800-255-7688**

Simu zinaweza kupigwa kwa siri na huduma za lugha zinapatikana.

www.justice.gov/ier | www.justice.gov/crt-espanol/ier

TTY 1-800-237-2515